**DAWA YAKO: Lisinopril ____ mg**

**<u>Kwanini ninapatiwa dawa hii?</u>** Una shinikizo la juu la damu. Shinikizo la juu la damu ni hatari iwapo halitotibiwa. Linaweza kusababisha viharusi na mishtuko ya moyo. Unaweza kupoteza maisha kwa kuwa na shinikizo la juu la damu ambalo halijatibiwa.

**Meza kidonge 1 mara tu baada ya kuamka.** Hauhitaji kula kitu kabla ya kumeza kidonge hichi.

**<u>Nitajihisije nitakapokunywa dawa hii?</u>** Nyakati nyingine, huwa kuna athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa dawa hii. Athari ya kimatibabu ni jambo lile unaloweza kujihisi ambalo si la kawaida. Baadhi ya athari za kimatibabu hutokea pindi mwili wako unapoanza kuizoea dawa hii na zinaweza kujumuisha kikohozi, kizunguzungu, maumivu ya kichwa, kichefuchefu na kuharisha.

Baadhi ya athari za kimatibabu huwa hazitokei mara nyingi, hatahivyo zinaweza kuwa kali sana. **Piga 911 au tembelea Chumba cha Dharura upesi kama utapata: mabaka ya ngozi; kuvimba kwa uso, mdomo, ulimi ama koo; kupata shida katika kupumua, kichefuchefu/kutapika kusikokoma; maumivu makali ya tumbo; mkojo mweusi.**

**<u>Nini kingine ninachopaswa kufahamu?</u>**

1. Unapaswa kunywa dawa hii kila siku hata pale utakapojihisi kuwa sawa.
2. Unapaswa kuijaza upya dawa hii kila mwezi.
3. Usinywe pombe. Kunywa maji mengi.
4. Kama utatembelea ofisi ya daktari tofauti, kliniki tofauti ya kitabibu ama chumba tofauti cha dharura, utapaswa kuwataarifu kwamba una shinikizo la juu la damu na kwamba unakunywa dawa ya Lisinopril.
5. Kama utashika ujauzito, utabidi kuacha kunywa dawa hii upesi. Rudi Kliniki ya Kitabibu ya Grace Village ili kumuona daktari, ili tuweze kukupatia dawa nyingine ya shinikizo la juu la damu ya wewe kunywa.

“Maudhui haya ni ya kwa makusudi ya utoaji taarifa pekee na hayapaswi kuhesabiwa kuwa kama ushauri wa afya wa kitaalamu. Daima tafuta kupata ushauri kutoka kwa Tabibu wako ama mhudumu mwingine wa afya mwenye sifa, kuhusiana na maswali yoyote unayoweza kuwa nayo yanayohusu hali fulani ya kiafya au matibabu.”